

MUHTASARI WA SERA

Wajibu wa Kimataifa, Uwajibikaji Ndani ya Nchi



Wito wa Kuboresha Ushirikiano wa Wadau katika Usimamizi wa Maliasili: Janga la Virusi vya Corona na mabadiliko ya hali ya hewa yamezidisha hali ya kuwa na mashaka, habari potofu na kutokuaminiana, hali ambayo inaweza kusababisha mizozo na usimamizi wa maliasili usio endelevu. Tunatoa wito wa usimamizi shirikishi na ukuzaji wa majukwaa shirikishi ili kuboresha uaminifu na ubadilishanaji wa habari.

Mnamo mwaka 2020 na 2021, janga la Virusi vya Corona na mabadiliko ya hali ya hewa vimesababisha na vimeongeza hali ya kuwa na mashaka kwenye mifumo yetu ya kijamii, kimazingira na kiuchumi. Vile vile, janga hili limetufanya tuwe na ufahamu zaidi juu ya utegemezi baina ya jamii na mazingira yetu. Athari kubwa zilizosababishwa na janga hili ulimwenguni zitahitaji juhudini mahususi kuhakikisha kunakuwepo na mpango jumuishi wa muda mrefu wa usimamizi wa maliasili.

Kuwa na mashaka husababisha kutokuelewana ambayo inaweza kuzusha mizozo kati ya wadau
Hii inaweza kutishia riziki za watu wanaotegemea rasilimali kwa kiasi kikubwa, kupunguza mapato ya serikali, na *mwishowe kusababisha matumizi ya maliasili yasiyo endelevu*.

Ushirikiano bora kati ya serikali, raia na taasisi zisizo za kiserikali katika usimamizi wa maliasili unakusudia kupunguza hali ya kuwa na mashaka na mizozo. Tunatoa wito wa uanzishwaji wa majukwaa jumuishi, ambapo wadau wanapewa nafasi ya kushiriki katika mijadala ya muda mrefu inayoweza kuboresha ubadilishanaji wa habari na kudumisha uaminifu kati yao. **Kulingana na matokeo ya utafiti, tunaangazia umuhimu wa mambo matatu katika usimamizi wa maliasili, ambayo ni:**

1. Michakato ya kushirikiana ambayo inawezesha ushiriki wenyе tija wa wadau **mbalimbali** (kama vile, raia na wawakilishi kutoka sekta tofauti, mashirika na mamlaka) ili kupunguza hali ya kuwa na mashaka. Katika usimamizi huo, wadau wanashirikiana pamoja

na wanafanya maamuzi kubuni michakato ya usimamizi. *Ni muhimu waandaaji na mashirika ya ufadhili katika michakato ya aina mbalimbali ya ushirikiano kutambua kwamba majukumu na haki za wadau mbalimbali ni lazima zifafanuliwe kwa uwazi na kukubalika pande zote ili kuepusha utoaji wa majukumu kutoka juu.*

2. **Majadiliano kati ya wadau yakifanyika kwa namna ambayo ni huru, ya uwazi na kukubalika yanaruhusu kupata habari kwa uwazi na upeanaji wa maarifa kwenye vyombo vya habari vya umma na kwenye tovuti rasmi na pia kupitia majukwaa wazi bunifu ya dijiti.** Majadiliano yenye tija, kama vile, kupendekeza pamoja chaguzi za sera, hupunguza habari potofu na kufafanua malengo ya matumizi ya rasilimali wakati pia inaimarisha uhusiano na kujenga uaminifu kati ya wadau kwa muda mrefu. *Mamlaka za serikali na watunga sera wanapaswa kutambua kuwa matumizi ya majadiliano ya majukwaa ya pamoja ya dijiti na yasiyo ya dijiti yanafanya kuwepo na mchakato bora Zaidi wa ufanyakaji maamuzi.*
3. **Kuimarisha ushiriki wa umma na jukumu la raia na jamii ni muhimu katika majadiliano na michakato ya ushirikiano.** Ushirikiano kati ya ngazi tofauti za mamlaka za serikali ni muhimu kukabiliana na mahitaji ya ndani ya nchi. Taasisi mbali mbali, mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya utafiti yanaweza kuwa ni waandaaji na wawezeshaji katika michakato hiyo ya ushirikiano. *Ni muhimu kutambua kwamba majadiliano yenye tija na juhudi za pamoja daima yanahitaji muda na kujitolea kwa wadau wote.*

MUHTASARI WA SERA

Wajibu wa Kimataifa, Uwajibikaji Ndani ya Nchi



Tangu mwaka 2012, utafiti wetu juu ya usimamizi wa maliasili nchini Ufini, Urusi, Msumbiji, Tanzania, Mexico na Indonesia umezingatia sana uhusiano kati ya wadau kutoka ngazi mbalimbali, ushiriki wa umma, na mikakati ya usimamizi wa maliasili.

University of Eastern Finland, Finland

Irmeli Mustalahti
Antti Erkkilä
Denis Dobrynin
Ida Herdieckerhoff
Virpi Pakarinen
Teppo Hujala

Eduardo Mondlane University, Mozambique

Almeida Sitoe
Jadwiga Massinga
Estêvão E. Chambule
Victorino Buramuge

College of Business Education, Tanzania

Edda Tandi Lwoga
Ubaldus J. Tumaini

Sokoine University of Agriculture, Tanzania

Dismas Lyegendili Mwaseba

University of Dar es Salaam, Tanzania

Aristarik Hubert Maro

National Autonomous University of Mexico, Mexico

Tuyeni Heita Mwampamba

Universitas Muhammadiyah Yogyakarta, Indonesia

Rijal Ramdani

University of Jyväskylä, Finland

Pekka Virtanen

Responsive Natural Resources Governance (RNRG) research group is funded by the Academy of Finland and the Finnish Strategic Research Council
irmeli.mustalahti(at)uef.fi

<https://sites.uef.fi/responsive-natural-resources-governance/>

